# KATIBA YA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WATU WENYE ULEMAVU TANZANIA

## (SHIVYAWATA)

(KAMA ILIVYOREKEBISHWA MWAKA 2008)

2008

# KATIBA YA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WATU WENYE ULEMAVU TANZANIA (SHIVYAWATA) YA MWAKA 2008

## UTANGULIZI

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasisitiza Uhuru, Haki na Usawa wa binadamu.Haki na usawa huu umezidi kutiliwa mkazo katika maazimio na mikataba mbali mbali ya Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Binadamu na Haki za Kiutu. Kundi la Watu wenye Ulemavu likiwa ni sehemu ya jamii, linastahili kikatiba kupata haki hizo zote kama ilivyo kwa makundi mengine ndani ya jamii.

Hata hivyo kulingana na vikwazo vinavyotokana na ama mazingira au mtizamo potofu ulioota mizizi ndani ya jamii, watu wenye ulemavu inawawia vigumu kupata haki hizo, kutambuliwa utu wao na kupewa fursa sawa.

Kwa muda mrefu jitihada nyingi zimekuwa zikifanywa na vyama mbalimbali vya watu wenye ulemavu katika kupigania haki, ustawi na maslahi ya watu wenye ulemavu unaohusiana na kila chama husika. Hata hivyo, ilionekana kuwa kutokakana na kila chama kuendesha harakati zake bila kuwa na ushirikiano wa moja kwa moja miongoni mwa vyama vya watu wenye ulemavu wa aina nyingine, kwa kiwango kikubwa vyama villikuwa vinashindwa kufanikisha malengo na matarajio ya kuanzishwa kwao. Hali hiyo ilisababishwa na kukosa nguvu na sauti ya pamoja na kukabiliana na vikwazo mbali mbali ikiwa ni pamoja na mtazamo potofu dhidi ya watu wenye ulemavu.

Kwa kuzingatia udhaifu uliojitokeza, vyama vitano vya watu wenye ulemavu vilivyokuwepo wakati huo ambavyo ni:-
Chama cha Walemavu Tanzania (CHAWATA)
Chama cha Wasioona Tanzania (TLB)
Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA)
Chama cha Maalbino Tanzania (CCMT) NA
Chama kwa ajili ya watu wenye Ulemavu wa Akili Tanzania (TAMH).

Vilikubaliana kuwa kiundwe chombo kimoja kiwakilishi chenye dhamana mbele ya vyombo vya serikali, jamii taasisi za kitaifa na kimataifa kwa niaba ya watu wenye

ulemavu wa aina zote hapa nchini. Wazo hilo lilizingatia ukweli kwamba umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

**Safari ya kufikia kuanzishwa kwa chombo hicho ilikuwa ndefu na hatimaye tarehe 10/8/1993 ilifikia kilele chake kwa kuzinduliwa rasmi Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA).**

Baada ya Shirikisho kuundwa, yalijitokeza matatizo mengi ya kiutendajiyaliyotokana na udhaifu wa kikatiba. Hivyo, ikaonekana kwamba palikuwa na umuhimu wa kuifanyia marekebisho katiba hiyo ili kuifanya SHIVYAWATA liendane na hali halisi iliyopo pamoja na kukidhi haja ya kuanzishwa kwake. Marekebisho ya katiba hii ya mwaka 2008 yamezingatia kanuni za Umoja wa mataifa juu ya haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu Duniani **zilizotangazwa kwenye Azimio namba 3447 la Umoja wa Mataifa lililopitishwa tarehe 9/2/1975**. Haya ni marekebisho ya kwanza kufanywa. Baada ya marekebisho, katiba ya SHIVYAWATA imekuwa na ibara tisa:-

1. Jina. Makao makuu, eneo, hadhi na nembo
2. Madhumuni
3. Majukumu
4. Uanachama
5. Muundo,
6. Uongozi
7. Fedha na mali
8. Lugha na njia za mawasiliano, na
9. Kuvunjika kwa SHIRIKISHO

**<u>MAANA YA SHIVYAWATA</u>**

Kwa mujibu wa katiba hii, SHIVYAWATA , maana yake ni muungano wa hiari wa vyama vya watu wenye ulemavu ,vya kwa ajili ya watu wenye ulemavu, na taasisi zenye nia na madhumni ya kulinda, kutetea na kuendeleza maslahi na haki za watu wenye ulemavu katika nyanja zote za maisha kama zilivyoainishwa katika katiba ya nchi. Kwa mujibu wa katiba hii SHIRIKISHO ni chombo cha msukumo

**<u>TAFSIRI YA ULEMAVU/MTU MWENYE ULEMAVU</u>**

Kwa maana na tafsiri iliyopo katika katiba hii ulemavu ni vikwazo na mapungufu ya uwezo wa kutumia na kumudu mazingira kwa ukamilifu au kiwango cha kawaida kama binadamu asiye na ulemavu bayana.

**<u>VYANZO VYA ULEMAVU</u>**

Baadhi ya vyanzo vya ulemavu ni:

1. ulemavu usababishwao na magonjwa kabla na /au baada ya kuzaliwa
2. ulemavu usababishwao na ajali,
3. ulemavu wa kurithi
4. ulemavu usababishwao na ulevi wa kupindukia na dawa za kulevya
5. ulemavu usabishwao na lishe duni, na
6. Ulemavu utokanao na uchafuzi wa mazingira au sababu nyinginezo

**<u>AINA ZA ULEMAVU</u>**

Baadhi ya aina za ulemavu ni;

1. Ulemavu wa kutoona
2. Ulemavu wa viungo
3. Ulemau wa akili
4. Ulemavu wa uziwi.
5. Ulemavu wa ualbino
6. Ulemavu wa otizimu, na
7. Ulemavu zaidi ya mmoja

## 1:0 JINA, MAKAO MAKUU, ENEO HADHI NA NEMBO

### 1.1 Jina

Jina litakuwa “Shirikisho la Vyama vya watu wenye Ulemavu Tanzania” kifupisho chake kitakuwa “SHIVYAWATA” na kwa kiingereza litajulikana kama “Tanzania Federation of Organizations of People with Disabilities.

1:2 **Makao Makuu:**

Makao Makuu ya SHIVYAWATA yatakuwa Dar es Salaam

1:3 **Eneo**:

Eneo la kufanyia kazi litakuwa Tanzania Bara.

1:4 **Hadhi**

a) SHIVYAWATA Kitakuwa ni chombo cha ngazi ya juu kabisa chenye kuuunganisha vyama kwa ajili ya watu wenye Ulemavu kwa lengo la kutetea, kulinda na kudumisha haki na maslahi ya jumla ya watu wenye ulemavu na hivyo kuwa na sauti ya mwisho kitaifa na kimataifa katika maslahi hayo.

b) SHIVYAWATA Itakuwa na haki ya kushtaki na kushtakiwa

1:5 **Nembo**

Mawimbi ni vikwazo katika harakati, mtumbwi huwakilisha jumuiya ya SHIVYAWATA, watu waliondani ni wanaharakati katika ukombozi wa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na wenye ulemavu na wasio na ulemavu na mnazi wa kijani ni ufukweni tuendako kwenye haki na maslahi.

**1.6 DIRA YA SHIVYAWATA**

Kuhakikisha kuwa jamii ya watanzania inatoa fursha sawa Kwa kila mtu mwenye ulemavu Kwa njia ya haki, kiutu na hadhi.

**1.7 MAARUBU (UTUME WA SHIVYAWATA)**

Kuendesha kampeni yenye michepuo itakayolenga kutokomeza ukandamizaji unaowakabili watu wenye ulemavu kwa njia ya mifumo ya kichumi kisasa na kijamii

2:0 **MADHUMUNI**

Madhumuni yatakuwa:-

a) Kuviunganisha vyama vya/kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa aina zote nchini ili kuviwezesha kuwa na sauti ya pamoja yenye nguvu ndani na nje ya nchi.
b) Kutia msukumo kwa serikali, chama kinachotawala, vyama vingine vya siasa na jamii kwa ujumla katika kutoa haki/ huduma wanazostahili watu wenye ulemavu kupitia vyama vyao.
c) Kusaidia Kwa kila hali kuanzishwa kwa vyama vya watu wenye ulemavu wenyewe na kuhakikisha ustawi na uhai kwa vile vilivyopo.
d) Kujenga uwezo wa Taasisi wanachama wa SHIVYAWATA na kutetea haki za watu wenye ulemavu kama ilivyo kwenye madhumuni ya vyama vyao na kuona kwamba vinafanikiwa kama ilivyokusudiwa.
e) Kushirikiana na chama kinachotawala, vyama vingine vya siasa, serikali pamoja na vyombo vingine vya jamii ndani na je ya nchi vyenye shabaha ya kuendeleza huduma za ustawi wa watu wenye ulemavu
f) Kuwa mshauri mkuu wa vyama wanachama.
g) Kuhakikisha kuwa serikali inatekeleza maazimio na mikataba ambayo imeridhia juu ya watu wenye ulemavu
h) Kuhakikisha uwepo wa uwakilishi wa watu wenye ulemavu katika vyombo vya maamuzi katika ngazi mbalimbali za serikali

3:0 **MAJUKUMU**

a) Kuunganisha na kuratibu shughuli za vyama vya / kwa ajili ya watu wenye ulemavu.
b) Kuwa msemaji mkuu wa mambo yote yanayogusa vyama / kwa ajili ya watu wenye ulemavu katika maslai ya jumla ndani na nje ya nchi.
c) Kupigania usawa wa fursa katika kupata haki za msingi kama zilivyoainishwa na matamko mbali mbali ya kitaifa na kimataifa juu ya watu wenye Ulemavu.
d) Kushirikiana na Tume / Vyombo vya haki za binadamu, katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu haki za watu wenye ulemavu.

e) Kufuatilia na kuhakikisha kwamba maamuzi mbali mbali yanayopitishwa na Serikali kuhusu watu wenye uelmavu yanatekelezwa ipasavyo.
f) Kutia msukumo ili kuhakikisha kwamba serikali inaridhia mikataba mbali mbali ya kimataifa kuhusu ustawi wa watu wenye Ulemavu.
g) Kupigania ushiriki wa watu wenye ulemavu katika vyombo vya maamuzi kuanzia ngazi ya chini mpaka ngazi ya Taifa na kimataifa.
h) Kupokea na kushughulikia masuala ambayo yameletwa na mwanachama kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.
i) Kuwa na haki ya kusuluhisha migogoro ya uongozi inayotokana na kukiuka katiba za vyama na migogoro mingine itakayojitokeza ndani ya vyama mwanachama.
j) Kujenga uwezo wa vyama au taasisi wanachama.
k) Kuteua wanasheria ambao watakuwa na majukumu ya kusuluhisha migogoro ya kikatiba itakayojitokeza katika shirikisho na vyama vyake.

## 4:0 **UANACHAMA**

### 4.1. Aina za uanachama

Kutakuwa na aina tatu za uanachama

Uanachama wa kawaida, uanachama wa kushirikishwa na uanachama wa heshima.

### 4.1.1 Uanachama wa kawaida:

Chama chochote cha kitaifa cha watu wenye ulemavu wenyewe au chama chochote Kwa ajili ya watu wenye ulemavu wasioweza kujisemea wenyewe kilichosajiliwa kwa ajili ya kuwasemea watu wenye ulemavu husika, kitakuwa mwanachama wa kawaida.

### 4.1.2 Uanachama wa kushirikishwa

Chama / Taasisi chochote / yoyote kilicho /iliyosajiliwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu tu kitakuwa /itakuwa mwanachama wa kushirikishwa.

### 4.1.3 Uanachama wa heshima

Taasisi yoyote itakayoteuliwa na Bodi baada ya kuridhika kuwa ina mtazamo sahihi kwa watu wenye ulemavu, na imefanya mambo ambayo yanalinda, yanaendeleza na yanatetea utu, haki na ustawi wa watu wenye ulemavu, itakuwa mwanachama wa heshima.

### 4.2 Sifa za kuwa Mwanachama

### 4.2.1 Uanachama wa kawaida

a) Chama ni lazima kiwe kimeundwa na watu wenye ulemavu wa aina hiyo kwa ajili ya kutetea haki na maslahi ya watu wenye ulemavu wa aina yao; au kimeundwa na wazazi / walezi wa watu wenye ulemavu wasioweza wenyewe.
b) Kiwe kimesajiliwa Kwa mujibu wa sheria.
c) Kiwe ni chama chenye hadhi ya kitaifa kwa mujibu wa katiba zao
d) Kiwe na Ofisi inayotambulika.

4.2.2 Uanachama wa kushirikishwa

a) Kiwe/iwe nia na madhumuni yake ni kuhudumia watu wenye ulemavu tu

b) Kiwe/iwe k/imesajiliwa kwa mujibu wa sheria
c) Kiwe/iwe k/imekwishafanya kazi si chini ya miaka mitatu
d) Kiwe/iwe na ofisi inayotambulika

**4.2.3 Uanachama wa heshima**

a) Awe ni mtu binafsi au taasisi inayotambulika kisheria.
b) Awe/ iwe na mtizamo sahihi kuhusiana na ulemavu wa watu wenye Ulemavu
c) Awe ni mtu binafsi au taasisi ambaye / ambayo amefanya / imeshafanya mambo yanaoonekana wazi wazi kuwa yanalinda, yanatetea au yanaendeleza utu, haki na ustawi wa watu wenye ulemavu nchini.

4:3. **Masharti ya Uanachama**

a) Kila mwanachama mpya isipokuwa kwa mwanachama wa heshima atatakiwa kuandika barua ya kuomba kujiunga na SHIVYAWATA ambayo itaambatanishwa na hati ya usajili na Katiba ya chama/taasisi. Maombi hayo yatajadiliwa na kutolewa maamuzi na kamati kuu ya SHIVYAWATA.
b) Akubaliane na vipengele vyote vilivyomo ndani ya katiba hii.
c) Atatakiwa kulipa kiingilio na ada ya mwaka kutegemeana na viwango vitakavyopitishwa na mkutano mkuu kwa wakati huo.

4**:4.1 Wajibu na haki za mwanachama**

Wajibu wa mwanachama

a) Kuwa tayari kutetea na kulinda malengo na madhumuni ya SHIVYAWATA kama yalivyo kwenye katiba hii.
b) Kutayarisha na kutuma taarifa ya utekelezaji wa kazi kwa SHIVYAWATA kila baada ya miezi 6.
c) Kuhudhuria ipasavyo vikao vianvyomuhusu kwa mujibu wa katiba hii.
d) Kusaidia kwa hali na mali ustawi wa maendeleo ya SHIVYAWATA.
e) Kulipa ada kama ilivyoainishwa katika katiba hii kipengele 4.3©
f) Kutoa michango mbali mbali kama itakavyolekezwa na SHIVYAWATA.

**4.4.2 Haki za mwanachama**

a) Kuhudhuria vikao vyote vya SHIVYAWATA vinavyomuhusu.
b) Kupata utetezi toka SHIVYAWTA pale inapobidi.
c) Kujitetea dhidi ya tuhuma yoyote inayomkabili
d) Kama hajaridhika na maamuzi yoyote yaliyotolewa dhidi yake na kikao chochote kukata rufaa kwenye vikao vya juu kwa kufuata ngazi zilizopo kwa mujibu wa katiba hii.
e) Kujiunga na vyama au mashirika ya kitaifa na kimataifa yanayomuhusu kufuatana na katiba yake bila kuingiliwa na SHIVYAWATA.
f) Kuwa msemaji wa mwisho juu ya masuala yanayomuhusu ndani ya SHIVYAWATA
g) Mwanachama atakuwa na haki ya kujiondoa katika uanachama
h) Haki ya kupata taarifa kutoka SHIVYAWATA
i) Haki ya kupata huduma kutoka kwenye SHIVYAWATA.

**4:5 Kukoma Uanachama**

Uanachama wa mwanachama utakoma endapo:-

a) Atashindwa kulipia ada ya uanachama kwa miaka miwili mfululizo.
b) Atavunja katiba ya SHIVYAWATA
c) Atajitoa kwa hiari yake mwenyewe kimaandishi.
d) Atakuwa amefutiwa usajili wake kwa mujibu wa sheria za nchi
e) Chama kikivunjika
f) Mwanachama wa SHIVYAWATA atakayejiunga na shirikisho/chama chochote/lolote kingine/lingine chenye/lenye kazi na madhumuni yanayofanana na SHIVYAWATA.

**4.6 Kurudishwa Uanachama**

a) Mwanachama atakayekuwa amejiuzulu au kujitoa, anapotaka kurudishiwa uanachama, atapaswa atumie na kufuata taratibu zote za kawiada kuomba uanachama kama mwanachama mpya.
b) Mwanachama atakayekuwa amefukuzwa uanachama kwa kuvunja katiba, hatarudishiwa uanachama kwa kipindi kisichopungua miaka miwili.Endapo atapenda kurudia uanachama atafuata taratibu zote za kawaida kama mwanachama mpya.

5:0 **MUUNDO WA SHIVYAWATA**

Mkutano mkuu,
Bodi
Kamati Tendaji
Jumuiya za SHIVYAWATA
Kamati za mikoa
Kamati za wilaya
Ofisi kuu tendaji
Idara mbalimbali

5:1:0 **Mkutano Mkuu**

a) Kutakuwepo na mkutano mkuu wa SHIVYAWATA ambao utafanya vikao vyake vya kawaida kikao kimoja kila baada ya miezi 30 (miaka miwili na nusu) lakini unaweza kufanya mkutano mkuu wa dharura kwa azimio la kamati tendaji ya SHIVYAWATA.
b) Taarifa ya mkutano mkuu itatolewa miezi mitatu kabla ya tarehe ya mkutano wa kawaida na mwezi mmoja kabla ya mkutano wa dharura.
c) Mwenyekiti wa mkutano mkuu atakuwa ni Mwenyikiti wa SHIVYAWATA na asipokuwepo makamu wake ataongoza. Iwapo wote wawili hawatahudhuria, mkutano utachagua mjumbe yeyote kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.
d) Kiwango cha wajumbe wanaohalalisha mkutano mkuu itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote halali wa mkutano mkuu kwa mujibu wa katiba hii.
e) Mkutano Mkuu utakuwa ndicho kikao kikuu cha SHIVYAWATA na ndicho kitakachokuwa na uamuzi wa mwisho juu ya masuala yote ya SHIVYAWATA.

f) Utakuwa na uwezo wa kuthibitisha, kubadili, kukataa au kubatilisha uamuzi wowote utakaotolewa na kikao chochote cha chini yake au kiongozi yeyote wa SHIVYAWATA.
g) Mkutano mkuu utakuwa na uwezo wa kubadili sehemu yoyote ya katiba ya SHIVYAWATA kwa uamuzi wa wajumbe wanaozidi nusu ya wajumbe walio na haki ya kupiga kura kwa mujibu wa katiba hii.

5:1:1 **Wajumbe wa Mkutano Mkuu**

Mkutano Mkuu wa SHIVYAWATA utahudhuria na wajumbe wafuatao:-

a) Wajumbe wote wa Bodi
b) Wajumbe wa Kamati tendaji
c) Mjumbe mmoja kutoka kila chama mwanachama mshirikishwaji.
d) Mjumbe mmoja kutoka taasisi mwanachama wa heshima.
e) Mjumbe mmoja SHIVYAWATA kutoka kila kamati ya kila mkoa.
f) Wajumbe wa nne kutoka chama mwanachama wa kawaida, wakizingatia usawa wa jinsia.

5.1.2 **Kazi za Mkutano Mkuu**

a) Utapokea na kujadili taarifa za kazi za SHIVYAWATA zitakazowasilishwa na kamati kuu na kutoa maelekezo au mipango ya utekelezaji wa shughuli za SHIVYAWATA kwa kipindi kitakachofuata.
b) Utachagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, mweka hazina na Wajumbe wanne wawili wakiwa wanawake miongoni mwa wagombea wawili kutoka kila chama mwanachama wa kawaida kwa kuzingatia uwiano wa jinsi na kupigiwa kura kwa kutenganisha uwiano huo watakaokuwa wajumbe wa Bodi na Kamati ya Utendaji.
c) Utapokea majina ya wenyeviti wa vyama kuingia katika Bodi na majina ya Makatibu wa vyama kuingia katika Kamati tendaji.
d) Utakuwa na uwezo wa kumfukuza kiongozi / mwanachama kwa mujibu wa katiba hii.
e) Utateua mwanachama wa heshina kwa mujibu wa ibara 4:3:1

**5:2:0 Bodi**

a) Kutakuwepo na Bodi ya SHIVYAWATA ambayo itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi (3). Inaweza kufanya mkutano usio wa kawaida wakati wowote inapolazimika.
b) Mwenyekiti wa SHIVYAWATA ndiye atakayekuwa mwenyekiti wa mikutano yote ya Bodi. Iwapo Mwenyekiti hatahudhuria Makamu Mwenyekiti ataongoza kikao, iwapo wote hawatahudhuria mkutano utachagua mjumbe yeyote kuwa mwenyekiti wa kikao hicho.
c) Itakuwa na wajibu wa kuangalia vitendo na mienendo ya wanachama na viongozi wa SHIVYAWATA. Endapo itaridhika kwamba tabia ya mwanachama au kiongozi wa chama, wa ngazi yoyote inamwondolea sifa za uanachama au za uongozi, itakuwa na uwezo wa kumsimamisha uanachama au uongozi katika ngazi yoyote ya uongozi wa SHIVYAWATA.

5:2:1 **Wajumbe wa Bodi**

Mkutano wa Bodi utahudhuriwa na wajumbe wafuatao:-

1. Mwenyekiti wa SHIVYAWATA
2. Makamu mwenyekiti wa SHIVYAWATA
3. Wenyeviti au wakuu wa vyama au taasisi wanachama wa kawaida wa SHIVYAWATA
4. Katibu mkuu wa SHIVYAWATA
5. Mweka hazina wa SHIVYAWATA
6. Wenyeviti/Wakuu wa Jumuiya.
7. Wajumbe wa nne wakuchaguliwa miongoni mwao angalau wawili wakiwa wanawake.
8. Mjumbe mmoja kutoka chama mwanachama mshirikishwaji atakaeteuliwa na Bodi.

5:2:2 **Kazi za Bodi**

a) Itaongoza mipango na shughuli zote za maendeleo ya SHIVYAWATA kama itakavyoamuliwa na kuagizwa na mkutano mkuu.
b) Itapokea na kujadili taarifa za utendaji za sekretariati za kila mwezi na za mwaka.
c) Itaitisha Mkutano Mkuu na kuandaa agenda zake.
d) Itajaza nafasi za uongozi zitakazokuwa zimeachwa wazi kutokana na sababu mbali mbali.
e) Itabadilisha uamuzi wa kikao chochote cha chini endapo haitaridhika na uamuzi huo.
f) Wakati wa uchaguzi itaunda kamati maalumu nje ya wajumbe wa kamati lakini ndani ya wajumbe wa mkutano Mkuu itakayochunguza na kufanya uteuzi wa hatua ya mwisho ya watu wanaoomba nafasi mbali mbali za uongozi, isipokuwa yale maamuzi ya Mkutano Mkuu.
g) Itakuwa msimamizi mkuu wa mali zaSHIVYAWATA
h) Endapo SHIVYAWATA itavunjika, itafanya maamuzi ya mwisho kuhusu milki ya mali na madeni dai/daiwa ya SHIVYAWATA kwa maslai ya watu wenye ulemavu
i) Itapokea na kujadili rufaa zote zitakazowasilishwa kwake ama na chama mwanachama au kiongozi atakayekuwa hajaridhika na maamuzi ya vikao va SHIVYAWATA dhidi yake, isipokuwa Mkutano Mkuu.

5:3:0 **Kamati Tendaji**

a) Kutakuwa na Kamati Tendaji ya SHIVYAWATA ambayo itakutana mara moja kila mwezi. Lakini inaweza kufanya mkutano wa dharura wakati wowote inapolazimika.
b) Itasimamia na kupanga taratibu za shughuli za kila siku za uendeshaji ofisi tendaji ya SHIVYAWATA.
c) Kamati tendaji ndicho kikao kitakachohusika na usimamiaji wa shughuli za kila siku chini ya maekelezo ya mkutano mkuu.
d) Itaunda kamati zingine ndogo ndogo za utekelezaji na kuandaa kanuni kwa kadiri itakavyoona inafaa.

e) Kuandaa kanuni za utendaji kazi kwa kamati za mikoa, wilaya na jumuiya za SHIVYAWATA katika ngazi mbalimbali

5:3:1 **Wajumbe wa Kamati Tendaji.**

a) Katibu mkuu wa SHIVYAWATA
b) Makatibu wa vyama/taasisi wanachama wa kawaida
c) Mweka hazina wa SHIVYAWATA
d) Makatibu wa Jumuiya.
e) Wajumbe wanne wakuchaguliwa wakiwemo wanawake wawili ambao pia ni wajumbe wa Bodi.
f) Kikao kinaweza kumualika mtendaji yeyote muajiriwa kama kuna umuhimu wa kufanya hivyo, isipokuwa hatokuwa na kura ya maamuzi.

5:3:2 **Kazi za Kamati Tendaji**

a) Kupitia na kuhakiki mapato na matumzi ya fedha za SHIVYAWATA
b) Kupokea na kuzifanyia kazi taarifa mbalimbali kutoka kwa wanachama.
c) Kuandaa agenda za vikao vya kamati kuu ya utendaji.
d) Kuandaa bajeti na mipango ya kazi ya utekelezaji wa SHIVYAWATA.
e) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa kanuni za uendeshaji wa ofisi ya SHIVYAWATA.
f) Itapokea, kujadili na kupitisha mapendekezo ya mikakati ya kimaendeleo itakayowasilishwa na ofisi kuu tendaji
g) Kuandaa taarifa za fedha na utekelezaji wa mipango mbali mbali ya SHIVYAWATA na kuiwasilisha kwenye kikoa cha kamati kuu
h) Kubuni mipango ya maendeleo
i) Kuandaa kanuni za fedha na za utendaji wa SHIVYAWATA
j) Kuandaa na kusimamia shughuli zote za utendaji wa SHIVYAWATA pamoja na Kanuni.

5:4:0 **JUMUIYA ZA SHIVYAWATA**

Kutakuwepo na Jumuiya mbalimbali za SHIVYAWATA.

5:4:**1 Jumuiya ya Wanawake na Watoto**

Kutakuwepo na Jumuiya ya wanawake na watoto ya SHIVYAWATA.

a) Jumuiya hii itayashughulikia masuala yote yanayowahusu wanawake na watoto wenye ulemavu katika SHIVYAWATA.
b) Itakuwa na mamlaka ya kuunda kanuni za uendeshaji wa shughuli za Jumuiya ikiwa ni pamoja na kufanya uchaguzi wa viongozi wake.

5:4:3 **Jumuiya ya Wazee**

Kutakuwepo na Jumuiya ya Wazee wa SHIVYAWATA.

a) Jumuiya hii itayashughulikia masuala yote yanayowahusu wazee wenye ulemavu katika SHIVYAWATA.
b) Itakuwa na mamlaka ya kuunda kanuni za uendeshaji wa shughuli za Jumuiya ikiwa ni pamoja na kufanya uchaguzi wa viongozi wake.

5:4:4 **Jumuiya ya Vijana**

Kutakuwepo na Jumuiya ya Vijana wa SHIVYAWATA.

a) Jumuiya hii itayashughulikia masuala yote yanayowahusu vijana wenye ulemavu katika SHIVYAWATA.
b) Itakuwa na mamlaka ya kuunda kanuni za uendeshaji wa shughuli za Jumuiya ikiwa ni pamoja na kufanya uchaguzi wa viongozi wake.

5:4:4 Jumuiya zote hapo juu kiutendaji zitawajibika kwa Kamati ya utendaji ya SHIVYAWATA.

5:5:0 **Ofisi kuu Tendaji**

Kutakuwepo na ofisi kuu tendaji itakayooongozwa na Mkurugenzi mkuu mtendaji ambaye ataajiriwa na atawajibika kwa kamati tendaji.

5:5:1 **Kazi za Ofisi kuu Tendaji/Mkurugenzi**

a) Itahusika na utendaji wa shughuli za kila siku katika ofisi ya SHIVYAWATA, ikiwa ni pamoja na kubuni na kutekeleza mikakati ya kimaendeleo ndani ya SHIVYAWATA.
b) Itafuatilia kutekeleza maazimio na maamuzi ya vikao mbali mbali vya SHIVYAWATA.
c) Itasimamia wajibu, haki, maslahi na shughuli za wafanyakazi wa ofisi tendaji.

5:6:0 **IDARA ZA SHIVYAWATA**

a) Kutakuwepo na idara mbalimbali za SHIVYAWATA kulingana na mahitaji.
b) Idara zote zitawajibika kwa Ofisi Kuu Tendaji ya SHIVYAWATA.

5:7:0 **Kamati za SHIVYAWATA**

**5.7.1 Kamati za mikoa**

a) Kutakuwepo na kamati ya kuratibu shughuli za SHIVYAWATA katika kila mkoa husika. Kamati hiyo itaundwa na watu wawili kutoka kila chama mwanachama wa kawaida na itakutana angalao mara mbili kila mwaka.
b) Inapofika wakati wa mkutano mkuu wa kitaifa, kila kamati ya mkoa itatoa mjumbe mmoja kuwakilisha.
c) Kamati za mikoa zitachagua viongozi wake katika nafasi ya mwenyekiti, katibu, mweka hazina na waliobaki watakuwa wajumbe wa kamati za mkoa.

5:7:2 **Kazi za kamati za mikoa**

a) Watatekeleza kazi zao kwa mujibu wa katiba na kanuni zitakazotolewa SHIVYAWATA Makao Makuu.
**b)** Kamati hizo zitakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano (5).

**5.8.0 Kamati za SHIVYAWATA za wilaya.**

a) Kutakuwepo na kamati ya kuratibu shughuli za SHIVYAWATA katika kila wilaya husika. Kamati hiyo itaundwa na watu wawili kutoka kila chama mwanachama wa kawaida na itakutana angalao mara mbili kila mwaka.

b) Kamati za wilaya zitachagua viongozi wake katika nafasi ya mwenyekiti, katibu, mweka hazina na waliobaki watakuwa wajumbe wa kamati za wilaya.

5:8:1 **Kazi za kamati za wilaya**

c) Watatekeleza kazi zao kwa mujibu wa katiba na kanuni zitakazotolewa SHIVYAWATA Makao Makuu.

**d)** Kamati hizo zitakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano (5).

6:0 **UONGOZI WA SHIVYAWATA.**

(a) Viongozi wa SHIVYAWATA watachaguliwa kwa kufuata kanuni zitakazoandaliwa na kamati tendaji na kuidhinishwa na Bodi kwa kuzingatia katiba hii.

(b) Mgombea katika nafasi kuu nne za juu kitaifa (mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu mkuu na mweka hazina) atahesabika ameshinda uongozi wa kupata idadi ya kura zinazomkubali kwa zaidi ya nusu ya idadi ya kura zote zilizopigwa. Kwa nafasi nyingine, wingi wa kura ndicho kitachokuwa kigezo.

(c) Kiongozi au mjumbe atakayechaguliwa na kuteuliwa kwenye ngazi yoyote ya uongozi wa SHIVYAWATA atadumu madarakani kwa kipindi cha miaka mitano.

(d) Kwa mujibu wa katiba hii kura zote za uchaguzi zitakuwa za siri.

6:1 **Sifa na masharti ya Uongozi.**

a) Kwa nafasi ya mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu mkuu na mweka hazina wa SHIVYAWATA, mgombea akiwa na cheo katika chama chake,akichaguliwa SHIVYAWATA, aache cheo katika chama chake mara achaguliwapo, na asiwe na wadhifa wowote unaolingana na vyeo vilivyotajwa katika ibara hii katika chama chake wakati wote akiwa kiongozi wa SHIVYAWATA na wala asiwe kiongozi mwandamizi serikalini.

b) Kiongozi aliyemaliza muda wake anaweza kuchaguliwa tena,lakini si kugombea zaidi ya awamu mbili katika nafasi ile ile .

c) Mgombea lazima atokane na chama ambacho uanachama wake ni wa kawaida na uongozi utakuwa ni wa kuzunguka katika vyama husika.

d) Awe na umri usiopungua miaka 25 katika ngazi zote za uongozi

e) Awe hajawahi kupatikana na hatia ya kosa lolote la jinai.

**6:2 Kuacha Uongozi**

Kiongozi wa SHIVYAWATA anaweza kuacha uongozi kwa:

a) Kuteuliwa kushika ngazi za kingozi mwandamizi maamuzi serikalini

b) Kujiuzulu kwa kuandika barua kwa kamati kuu ya SHIVYAWATA.

c) Kuondolewa na mamlaka husika

d) Chama chake kufutiwa usajili na msajili wa vyama na

e) Kifo

f) Kupatikana na kosa la jinai

g) Kufukuzwa na chama chake

6:3 **Viongozi wakuu wa SHIVYAWATA**

Kutakuwepo na viongozi wakuu wa SHIVYAWATA wafuatao:

a) Mwenyekiti
b) Makamu mwenyekiti
c) Katibu mkuu, na
d) Mweka hazina

6:4 **Kazi za viongozi wakuu wa SHIVYAWATA.**

6:4:1 **Mwenyekiti**

a) Atakuwa ndiye msemaji mkuu wa SHIVYAWATA.
b) Atakuwa msimamizi mkuu wa SHIVYAWATA.
c) Atakuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya Bodi na Mkutano Mkuu
d) Kura zitakapolingana, Mwenyekiti atakuwa na kura ya turufu.

6:4:2 **Makamu Mwenyekiti**

a) Atamsaidia mwenyekiti katika shughuli zake za kila siku .
b) Mwenyekiti anapokuwa hayupo Makamo atasimamia badala yake.

6:4.3 **Katibu Mkuu**

a) Atakuwa msimamizi mkuu wa kazi za SHIVYAWATA
b) Ataitisha vikao vyote vya SHIVYAWATA kwa kushauriana na mwenyekiti
c) Atatunza kumbukumbu zote za SHIVYAWATA pamoja na shughuli za kamati za Mikoa, kwa kushirikiana na Mhazina pamoja na Mkurugenzi.
d) Atakuwa mwenyekiti wa vikao vyote vya sekretarieti na endapo hayupo wajumbe watachagua mwenyekiti
e) Ataratibu shughuli zote za SHIVYAWATA
f) Atawajibika kwa Kamati Tendaji, Bodi na Mkutano Mkuu.

6:4:4 **Mweka hazina**

a) Atabuni mipango ya Maendeleo, fedha na uchumi ya SHIVYAWATA kwa kushirikiana na Mkurugenzi mtendaji na Mhasibu chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu.
b) Atakuwa msimamizi wa fedha na mali zote za SHIVYAWATA ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi.
c) Atawajibika kwa Kamati Tendaji, Bodi na Mkutano Mkuu.

6:5 **Miiko ya viongozi**

Ni mwiko wa kiongozi wa SHIVYAWATA

a) Kupokea au kutoa rushwa.
b) Kupata mapato kwa njia ya kificho
c) Kuchochea vurugu katika SHIVYAWATA na vyama wanachama.
d) Kuiba mali ya SHIVYAWATA
e) Kuwa mlevi wa kupindukia
f) Kutumia jina, fedha au mali ya SHIVYAWTA kwa manufaa binafsi.
g) Kuhujumu au kusaliti SHIVYAWATA kwa manufaa binafsi au taasisi fulani

**7:0 FEDHA NA MALI ZA SHIRIKISHO**

7:1 **Mapato**

Mapato ya SHIVYAWATA yatatokana:

a) Viingilio, ada na michango ya wanachama
b) Michango toka serikalini na misaada toka wakala wa hiari wa ndani na nje ya nchi
c) Miradi ya uzalishaji au vitega uchumi vitakavyokuwa vimeanzishwa na SHIVYAWATA.

**7:2 Matumizi**

a) Mapato ya fedha za SHIVYAWATA yatatumika kulianga na madhumuni yaliyo kwenye katiba hii.
b) Kwa matumizi yoyote, lazima taratibu imara za udhibiti wa mahesabu ziwe zimetoshelezwa kikamilifu kama zitakavyowekwa na Kamati Tendaji, kwa sheria/ taratibu za kifedha za SHIVYAWATA na kimataifa

**7:3 Ukaguzi**

a) Ukaguzi wa fedha za SHIVYAWATA utafanywa na mkaguzi aliyesajiliwa atakayeteuliwa na Kamati Tendaji ya SHIVYAWATA na kwa mujibu wa taratibu za SHIVYAWATA
b) Kila mwaka ukaguzi wa mapato na matumizi ya mali za SHIVYAWATA utafanywa na mkaguzi wa nje.
c) Taarifa ya ukaguzi itawasilishwa kwenye kikao cha mwaka cha sekretarieti
d) Ikibidi, ukaguzi wa dharura unaweza kufanyika wakati wowote.

**8:0 LUGHA NA NJIA ZA MAWASILIANO**

8:1 Lugha

Lugha itakayotumika katika kuendeshea shughuli za SHIVYAWATA itakuwa Kiswahili, kiingereza, lugha ya alama, nukta nundu, na lugha ya alama ya kupapasa

8:2 **Mawasiliano**

Maandishi ya kawaida, mandishi yaliyokuzwa, maandishi ya nukta nundu pamoja na nyenzo nyinginezo zitakuwa ndio njia ya mawasiliano.

9:0 **KUVUNJIKA KWA SHIVYAWATA.**

Endapo SHIVYAWATA itavunjika, Bodi itakuwa na uamuzi juu ya mali na madeni ya SHIVYAWATA wakishauriana na vyama wanachama.

Imesainiwa na kuwasilishwa leo tarehe 23 Mwezi Machi, 2009 na

……………………………

Felician Mkude
**KATIBU MKUU**
**SHIVYAWATA**